TAARIFA MBALIMBALI TOKA IDARA YA ELIMU MSINGI – JANUARI, 2019

1.0. UTANGULIZI:

Idara ya Elimu Msingi ni miongoni mwa Idara 13 zilizopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Idara hii ina lengo kubwa la kuhakikisha inasimamia utoaji wa elimu bora ya Elimu ya Msingi na Awali kwa watoto wanaostahili kupata elimu hiyo pamoja na Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na Elimu ya Watu Wazima.

Kwa mwaka 2018 idara imesimamia shughuli mbalimbali ambazo zimesaidia kuboresha taaluma hasa kuongeza ufaulu katika Mitihani ya Kitaifa kama itakavyoonyeshwa hapo chini. Mwaka huu 2019, idara imejipanga tena kusimamia ufundishaji na kuhamasisha wananchi kujitolea kuongeza miundombinu kwenye shule ili wanafunzi wapate elimu kwa viwango vinavyokubalika.

2.0. SHUGHULI ZILIZOFANYIKA NA ZINAZOTARAJIA KUFANYIKA MWAKA 2019.

2.1. Michezo kupitia Shirika la Jambo Bukoba.

- Bonanza la michezo ngazi ya wilaya lilifanyika wilayani tarehe 30.11.2018. Shule zilizoshiriki ni Mugoma, Murutabo, Remela na Katerere.
- Katika michezo hiyo Shule ya Msingi Mugoma ilipata ushindi wa kwanza na Shule ya Msingi Remela ilipata ushindi wa pili. Shule zote mbili zitapata Shs 8,000,000/= ambapo kila shule itapata Shs.4,000,000/=. Kamati za Shule zitapendekeza ni miradi ipi itatekelezwa kupitia fedha hizo (*mfano, Darasa au matundu ya vyoo*). Jamii itachangia 25% kwenye miradi hiyo.

3.0. MATOKEO YA MITIHANI YA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI, 2018.

- Wanafunzi **4460** (Wav 2,370 na Was **2,696**) sawa na asilimia ***88.05*** ya wanafunzi waliofanya mtihani walifaulu. Wanafunzi **997** sawa na asilimia ***11.95*** hawakufaulu.
- Wanafunzi **4,186** (Wav **1996** na Was **2190**) walipangwa kuendelea na masomo ya Sekondari katika shule za kutwa **23**. Wanafunzi **18** (Wav **12** na Was **6**) wamepangwa shule za vipaji, ufundi na bweni kawaida.
- Wanafunzi **256** (Wav **90** na Was **166**) hawakupata nafasi kutokana na ukosefu wa vyumba vya madarasa. Awali wanafunzi hao walipangwa katika shule zifuatazo: Rusumo B (**33**), Nyakisasa (**50**), Ngara (**62**), Murgwanza (**23**), Mugoma (**23**), Mabawe (**49**), Kanazi (**26**).

4.0. MIKAKATI:

Ili kuhakikisha wanafunzi **256** waliobaki wanaendelea na masomo pamoja na kuhakikisha tatizo hilo halijitokezi mwaka 2020 ambapo vitahitajika vyumba **70** (wahitimu wanatarajia kuingia Kidato cha I 2020 ni **5,072**). Wilaya imejiwekea mikakati ifuatayo:-

4.1. **<u>Mikakati ya muda mfupi</u>**:

- Kuhakikisha wananchi wanashirikiana kujenga vyumba vipya 6 vya madarasa vinavyohitajika kwa sasa ili vikamilike ifikapo tarehe 30.03.2019. Halmashauri imetenga Shs. 24,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa mabati, saruji na nondo kwa ajili ya madarasa hayo.
- Wanafunzi **23** walibakia katika Sekondari ya Mugoma, wazazi wao wameshauriwa kuomba nafasi zilizo wazi katika shule ya sekondari ya Muruvyagira.

4.2. **<u>Mikakati ya muda mrefu</u>**:

- Kuhakikisha kila Kijiji kinakusanya vifaa mfano mawe, mchanga na matofali 300,000 kwa ajili ya kuanza kujenga vyumba vya madarasa 2 kwenye shule ya sekondari ya Kata na kwenye shule ya msingi iliyopo kijijini hapo.
- Kuhakikisha shule mpya ya Mumiterama inasajiliwa kabla ya mwezi Agosti, 2019 ili iweze kupokea wanafunzi mwaka 2020. Kwa sasa shule hiyo ina vyumba sita. Majengo yanayotarajiwa kujengwa ni jengo la Utawala, Maabara 3, matundu ya vyoo 6 na nyumba ya Mkuu wa Shule.

5.0. MATOKEO YA UPIMAJI WA DARASA LA NNE.

Wanafunzi **7,598** walisajiliwa kufanya mtihani (Was **3711** na Wav **3619**). Wanafunzi **7,733** (Was **3711** na Wav **3619**) walifanya Upimaji. Wanafunzi **7212** (Was **3669** na Wav **3543**) sawa na asilimia ***98.39*** walifaulu Upimaji. Halmashauri ilishika nafasi ya **22** kati **186**.

6.0. UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI WA ELIMU YA AWALI NA MSINGI.

- Wanafunzi **11,973** (Wav **6254** na was **5719**) wanatarajia kuanza Darasa la Awali na wanafunzi **11,157** (Wav **5431** na was **5726**) wanatarajia kuanza Darasa la Kwanza mwaka 2019. Wanafunzi hao wanahitaji miundo mbinu stahili ili waweze kumudu masomo yao ipasavyo. Hadi tarehe 14.01.2019 (siku saba shule zifunguliwe takwimu zinaonyesha wanafunzi **7,687** (Wav **3902** na Was **3785**) Wameandikishwa Darasa la Awali sawa na **64** ya wanaotarajiwa wanafunzi **9662** (Wav **4564** na was **5098**) sawa na asilimia **87** wameandikishwa kuanza Darasa la Kwanza.
- Kufikia Desemba, 2018 Idara ilikuwa na Upungufu wa miundo mbinu kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini hivyo kutokana na ongezeko hili la Uandikishaji ni wazi kuwa upungufu huo wa miundombinu utaongezeka.
-

S/N	Miundombinu	Mahitaji	% Yaliyopo	Iliyopo	Upungufu	% Upungufu
1	Vyumba vya madarasa	1869	810	43	1059	56
2	Nyumba za walimu	1455	248	17	1207	82
3	Matundu ya vyoo	3785	1010	27	775	20
4	Ofisi za walimu	264	13	5	251	95

7.0. MIKAKATI YA KUPUNGUZA UPUNGUFU WA MIUNDOMBINU KWENYE SHULE ZA MSINGI:

Tatizo la upungufu wa miundo mbinu linaongezeka kila mwaka kutokana na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi kwenye madarasa ya Awali na Darasa la Kwanza. Hii ni kutokana na mwamko mkubwa wa wazazi kuandikisha watoto wa shule kupitia mpango wa **Elimu Bila Malipo**.

Halmashauri ya Wilaya inawapongeza sana wadau wa Elimu na watu binafsi wanaojitolea kujenga miundo mbinu kwenye shule zetu. Wadau hao ni kama Tumaini Fund, Kabanga Nickel, Jambo Bukoba, TCRS, NMB na watu binafsi mfano Dr Sikubwambo Ngendabanka kuwataja kwa uchache.

7.1. Mikakati iliyopo:

- Kuendelea kutumia makusanyo ya ndani kugharimia vifaa vya viwandani kwa ajili ya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.
- Kushirikisha Mheshimiwa Mbunge kuchangia ujenzi wa miundo mbinu kupitia fedha za mfuko wa Jimbo.
- Kuendelea kuweka kwenye bajeti maombi ya fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu.
- Kuendelea kuwaomba wadau mbalimbali kutujengea miundo mbinu kadri watakavyoweza.

8.0. MIUNDOMBINU INAYOTARAJIA KUJENGWA 2019.

Ili kukabiliana na upungufu wa miundo mbinu kwenye shule za msingi, wadau mbalimbali, mfuko wa Jimbo na wananchi kwa ujumla wameanza ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo kwenye maeneo yao.

Aidha kupitia mradi wa LADP (*Local Area Development Programme*) Halmashauri itajenga miundo mbinu kwenye shule tatu za msingi. *Jedwali hapo chini linaonyesha miradi itakayogharimiwa kupitia mpango wa LADP, Mfuko wa Jimbo na Wananchi:-*

NA	AINA YA MRADI	SHULE	MAELEZO
1.	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi.	Murukulazo	Vyumba vinaendelea kujengwa na Dr Ngendabanka wa Kijiji cha Murukulazo kwa gharama zake
2.	Ujenzi wa miundo mbinu kupitia mradi wa LADP	Makugwa	Vyumba 5 vya madarasa Jengo 1 la Utawala Nyumba 1 ya Mwalimu Matundu 12 ya vyoo Madawati na viti
3.	Ujenzi wa miundo mbinu kupitia mradi wa LADP	Ngoma	Vyumba 3 vya madarasa
4.	Ujenzi wa miundo mbinu kupitia mradi wa LADP	Rusumo	Vyumba 5 vya madarasa Jengo 1 la Utawala Nyumba 1 ya Mwalimu Matundu 12 ya vyoo
5.	Chumba kimoja cha darasa na Ofisi ya Mwalimu Mkuu	KABANGA	Msingi umekamilika.
6.	Vyumba viwili vya Madarasa.	NGUNDUSI	Kuna mawe tripu tano (5), Tofali tripu nne (4) na mchanga tripu tano (5).
7.	Choo ya Walimu	NZAZA	Shimo limekamilika.
8.	Vyumba viwili vya madarasa	DJURULIGWA	Mawe tripu 3, Mchanga tripu 2
9.	Vyumba viwili vya madarasa	RULENGE	Msingi umekamilika.
10.	Vyumba viwili vya madarasa	NYANZARI	Boma limefikia hatua ya madirisha.
11.	Ujenzi wa chumba kimoja cha darasa	GOYAGOYA	Mawe tripu 4.
12.	Vyumba viwili vya madarasa	KIHINGA	Mawe tripu 10, Mchanga tripu 10, Tofali tripu 4
13.	Chumba kimoja cha darasa	MURUTABO	Msingi umekamilika.
14.	Ujenzi wa choo	KIRUSHYA	Tofali trip 2, Mchanga tripu 3 na Kokoto tripu 2.
15.	Vyumba viwili vya madarasa	MURUGUNGA	Bati limeezekwa.
16.	Chumba kimoja cha darasa	NTANGA	Hatua ya renta.
17.	Ujenzi wa choo	MURUSAGAMBA	Shimo limekamilika.
18.	Chumba kimoja cha darasa	NYAMAHWA	Mawe tripu 3 na Mchanga tripu 1.
19.	Matundu 8 ya vyoo	KASHINGA	Shimo limekamilika.
20.	Nyumba ya Mwalimu	NYANKENDE	Mawe tripu 4 na Mchaga tripu 4.
21.	Vyumba viwili vya madarasa	MUMITERAMA	Hatua ya renta
22.	Ujenzi wa vyoo	MUGASHA	Shimo limechimbwa.
23.	Ujenzi wa vyoo	KUMUYANGE	Shimo limechimbwa.

NA	AINA YA MRADI	SHULE	MAELEZO
24.	Vyumba viwili vya madarasa	MAYENZI	Mchanga tripu 3, mawetrpiu 6, fedha taslimu 1,200,000
25.	Chumba kimoja cha darasa	KUMUTANA	Kokoto tripu 5, Mawe tripu 9,Mchanga tripu 10 na Tofali tripu 2.
26.	Vyumba viwili vya madarasa	KUMUNAZI	Tofali trpu 5, Mawe tripu 3
27.	Chumba cha darasa na Ofisi ya walimu	KAPFUHA	Hatua ya renta chumba cha darasa, Ofisi ya walimu msingi umekamilika.
28.	Chumba cha darasa	KABAHESHI	Mawe tripu 5.
29.	Chumba cha darasa	KAGALI	Msingi umekamilika.
30.	Ujenzi wa choo matundu 8	NYAKIZIBA	Shimo limechimbwa, kokoto tripu2 na mchanga tripu 2.
31.	Ujenzi wa choo matundu 12	MURUKAGATI	Matundu 6 yamekamilika kujengwa, mchanga tripu 1na mawe tripu 1.
32.	Ujenzi wa choo matundu 8	CHIVU	Boma limeezekwa.
33.	Ofisi ya walimu	NYABIHANGA	Hatua ya renta
34.	Vyumba viwili vya madarasa	RUBANGA	Bati limeezekwa.
35.	Ofisi ya Walimu	MUBWILINDE	Hatua ya boma
36.	Vyumba 3 vya madarasa	MUKIREHE	Boma limeezekwa.
37.	Ujenzi was too ya chakula	MUKIBOGOYE	Hatua ya renta.
38.	Ujenzi wa choo ya walimu	KANAZI	Tripu 1 tofali na mchanga tripu 1.
39.	Chumba cha darasa	MUKIDIDILI	Mawe tripu 5, tofali tripu 3, mchanga tripu 2 na kokoto tripu 1.
40.	Ujenzi wa choo matundu 6	MUBINYANGE	Shimo limechimbwa.
41.	Ujenzi wa choo matundu 6	SHANGA	Shimo limechimbwa.
42.	Ujenzi wa choo matundu 6	MUBUHENGE	Shimo limechimbwa.
43.	Ujenzi wa chumba cha darasa	RUSENGO	Fedha taslimu 1,600,000.

9.0. MAPOKEZI YA FEDHA ZA ELIMU BILA MALIPO:

Halmashauri imeendelea kupokea fedha za Elimu Bila Malipo kila mwezi. Kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Novemba, 2018 Halmashauri imepokea Shs. **316,426,000.00** Katika mchanganuo ufuatao:-

- Ruzuku ya Uendeshaji wa shule Shs. 173,926,000.00
- Posho ya madaraka kwa walimu wakuu Shs. 115,000,000.00
- Posho ya madaraka kwa Maafisa Elimu Kata Shs. 27,500,000.00

10.0. UANZISHAJI WA SHULE MPYA MWAKA 2019.

Kwa lengo la kusaidiana na Serikali kutoa elimu kwa watoto waliofikia umri wa kuanza shule, Masista wa Kanisa Katoliki wa Jimbo la Rulenge – Ngara wameanzisha shule ya Msingi na Awali iitwayo **St. Boneventure English Medium Primary School** yenye usajili Na. **17743.** Shule hiyo ipo katika kijiji cha Mumiterama Kata ya Nyamiaga.

Aidha shule nyingine mpya iitwayo **Wisdom English Medium Primary School** imeanzishwa na Bw. Rwechungura Simeon John. Shule hiyo yenye namba za Usajili **17699** ipo katika kijiji cha Kumunazi kata ya Kasulo.

Kwa ujumla ongezeko la shule **2** mpya limeongeza idadi ya shule za msingi kwenye Halmashauri kuwa **121**. Wanafunzi wapatao **200** watapata fursa ya kupata elimu kupitia shule hizo.

Pamoja na shule hizo za watu/ mashirika binafsi Halmashauri inaendelea na utaratibu wa kukamilisha shule mpya katika kijiji cha Mukubu itakayoitwa Makugwa Shule ya Msingi. Tayari shule hiyo ina madarasa manne na matundu 12 ya vyoo yaliyojengwa na Kabanga Nickel. Shule nyingine zinazoendelea kujengwa na wananchi ni Misenani (Kata ya Murusagamba), Nyamikono (Kata ya Rusumo Kijiji cha Mshikamano) na Gashaza (Kata ya Muganza Kijiji cha Mukalinzi). Ni imani ya Halmashauri kuwa kukamilika kwa shule hizo kutapunguza msongamano kwenye shule zilizopo kwenye Vijiji husika pamoja na kuwapunguzia watoto mwendo mrefu wa kutembea kufikia shule mama.